

Tumtazame Mungu ili kutunza mazingira

Na Mchg. Thomas Maumbuka

Ni jukumu la Nani kutunza mazingira? “Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu akamweka katika bustani ya Edeni ailime na kuitunza,” (Mwanzo 2: 15). Mazingira yana mchango mkubwa katika afya ya mwanadamu maana kuna uhusiano wa mti na mwanadamu. Mstari wa 29 tunasoma: “Tazama nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi”.

Baada ya kupewa bustani tumeitumia vibaya kwa kuharibu badala ya kutunza. Nimetembelea Mbuga za Wanyama kadhaa hapa nchini kama vile Ngorongoro, Tarangire, Manyara, Serengeti na Mikumi. Katika maeneo hayo mazingira yanatunzwa vizuri sana, ndiyo ‘Eden’ anayoisema Mungu.

Kuna aina mbalimbali za wanyama, ndege na maji ya kutosha. Hivyo ni kivutio kwa watalii na ndio sababu wameweka tozo ya lango ukifika unalipia ada kwa kupita katika mbuga. Hata hali ya hewa ni tofauti maana jua linapoozwa na misitu.

Macho yetu hayamtazami Mungu ndio maana uharibifu huu umeongezeka. Kwa mfano katika Wilaya ya Kishapu, Shinyanga kuna ukame sana. Kutotunza mazingira kunaharibu pia imani, upendo, furaha, afya, nk. Jinsi ya kutunza mazingira Rais wa awamu ya tano aliagiza watu wasafishe mazingira na watu wakatoka kwa wingi kufanya usafi wa maeneo yao na maeneo mengine kama masokoni, hospitalini na katika barabara za mijini.

Lakini tusingoje mpaka hali iwe mbaya ndipo mtu atukumbushe kutunza mazingira. Yapo mambo matano yanayoweza kusaidia uweze kutunza mazingira. Jambo la kwanza, tukubali siku zote kuwa tayari kupokea wajibu wa kutunza mazingira ya kimwili na kiroho. Pili tujiandae kwa wajibu huo kwa mfano Musa aliandaliwa alipoambiwa “vua viatu” vyako kabla ya kupewa wajibu wa kuwakomboa wana wa Israeli.

Daudi kabla ya kupambana na Goliathi aliandaa kombeo na hata Esta alifunga na kuomba kwa ajili ya watu wake. Tatu inabidi kutambua kwamba ziko changamoto utakazo kumbana nazo lakini wewe umtazame Bwana wala usiogope.

Fanya uliyojipangia kufanya kwa bidii. Usimwangelie mtu, mtazame Bwana. Jambo la nne ni kuwa tayari kulipa gharama. Mfano, Musa alifika mbele ya Farao na kumwambia awaache wana wa Israeli waondoke bila kuogopa kwamba angeweza kufa. Esta aliingia kumwona Mfalme kinyume na utaratibu na hakujali kwamba angeweza kuangamia. Wote hawa walimtazama Bwana hata kama mazingira ya uhai wao hayakuwa salama.

Hitimisho na jambo muhimu kuliko yote ni kujiuliza unataka kufanya nini ndipo uweke mpango kama vile kupanda miti, kufanya usafi wa mazingira, kuhimiza wengine wapande miti na mwisho ujipime katika hayo.